# Learning by Ear 2009

## Media & Information

## Author: Hope Azeda

## Redaktion: Ludger Schadomsky

## Kisuaheli Translation:Eric Ponda

### EPISODE 4

| ***CHARACTERS*** | |
|---|---|
| **Announcer:** | **Male/female** |
| **“Young Junior”** | **Male, 15 years old** |
| **“Sister P.”** | **Female, 16 years old** |
| **“Charlie”** | **Male, 18 years old** |
| **“Ezra”:** | **Male, 22 years old. Brother to “Young Junior”.** |
| **Student** | **Young male** |

**INTRO**

Hujambo msikilizaji na kwa mara nyingine karibu kwa makala yetu ya Learning By Ear “Noa Bongo jenga maisha yako” tukizungumzia sekta ya habari na Vyombo vya habari. Hivi leo wahusika katika kipindi hiki wanamtembelea kakake

Young Junior, Ezra anayesomea uandishi wa habari katika chuo kikuu na pia kufanya kazi katika kituo cha redio chuoni humo ili kupata uhauri.Hebu tusikilize ni ushauri gani atakaowapa wanahabari hawa chipukizi kuhusiana na ndoto yao ya kuanzisha kituo cha redio.

**SCENE ONE**

***At the university halls of residence, there are people walking on concrete floors, door opening and closing.***

**SFX footsteps on the floor.**

**1. Young J:** Mtazame Sister P.

**2. Sister P:** Eh, kwanini mnanitazama hivyo?

**3. Young J:** Kwasababu ya ulivyovalia kama JIO!. Mtu anaweza kukufananisha na mmoja wa wanafunzi chuoni hapa. Ndio sababu ya kuchelewa?

**4. Sister P:** Samahani lakini hilo haliwezi kutusaidia. Lengo kubwa la kuja hapa ni kumtafuta Ezra au sivyo? Je mnajua chumba anamokaa? Umewahi kufika chuoni mbeleni au tunababahatisha? Tuseje tukakamatwa na maafisa wa usalama kwa kuingia hapa bila ruhusa.

**5. Young J:** Ndio.. nimewahi kufika wakati nilipomuleta kakangu mara ya kwanza, bado nakumbuka vizuri sana baada ya kupanda hizi ngazi tulipindukia kushoto.

**6. Charlie:** Milango yote imewekwa nambari.Je unaweza kukumbuka ni mlango upi?

**7. Young J:** Hebu twendeni chini hapa. Hasa …! Upande wa kulia. Er, ehhe sasa ni mlango unaofuatia. Hasa mlango ni huu hapa.

**8. Sister P:** Tubishe ?

| **SFX Knocks on the door.** |
| --- |

**9. Student:** Pita ndani kama wewe ni Mrembo!

**10. Sister P:** Ohoooo ….Goosh!

**11. Charlie :** Pita ndani, mrembo!

**12. Sister P:** Funga mdomo wako.

| **SFX Knocks again. Door opens** |
| --- |

**13. Student:** Naam, nimsaidie na nini?

**14. Young J:** Habari gani, tunamtafuta Ezra.

**15. Student:** Ezra? Mumekosea hayupo chumba hiki. Ni mwanafunzi wa mwaka wa ngapi na anasomea nini?

**16. Young J:** Ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu na anasomea uandishi wa habari.

**17. Student:** Sawa, wanafunzi wa mwaka wa tatu wako katika jingo lile linaloangaliana na hili. Jengo hili ni la wanafunzi wageni kabisa, yaani wanafunzi wa mwaka wa kwanza.

**18. Sister P:** Kwani usimpigie simu?

**19. Charlie:** Wazo zuri sana.

**20. Student:** Kwaherini .

**SFX closes door**

**21. Young J:** Hallo, Hallo huyo ni Ezra?

**SFX Phone voice**

**22. Ezra:** Naam…. Young J, habari gani? Nimekusubiri hadi nikachoka.

**23. Young J:** Bwana wee, tuko hapa chuoni tumepotea njia, uko wapi wewe?

**24. Ezra:** Niko katika studio za redio ya chuo kikuu. Mnaweza kumuuliza mtu yoyote, atamuonyesha mahali studio zilip.Fanyeni haraka maana nitaingia studioni katika katika muda wa sekunde chache zijazo.

**25. Young J:** Sawa. Hizi ni habari njema ,kwani sio tu kumkuta Ezra na kushauriana naye kuhusu mpango wetu bali pia fursa ya kutembelea na kujionea mambo yalivyo studioni.

**26. Charlie:** Na pia nimebeba nakala ya Album yetu kwa hivyo tunaweza kumuuliza kama atakubali kuicheza studioni.

**27. Sister P:** Twendeni upesi.

**END OF SCENE TWO**

**SCENE THREE**

***At the radio station, the atmosphere is calm with soft music in the background.***

| |
|---|
| **SFX** ***Rattling and opening bottles of soda***. |

**28. Ezra:** Karibuni mjisikie huru.

**29. All:** Asante.

**30. Ezra:** Nitarudi studioni katika muda wa dakika 30 kuendelea na kipindi changu, kwa hivyo kabla ya

wakati huo,tunaweza kuendelea na mazungumza, yaliywaleta hapa.Je mnataka kutembelea studio zetu au tuendelee na mazungumzo.

**31.Young J:** Dunno. Tuzingatie yaliyotuleta kwanza kisha mambo mengine baadaye.

**32. Sister P:** Ezra, tunapanga kuanzisha kituo cha redio ya jamii, lakini tunahitaji ushauri wako kuhusiana na suala hili, na ndio sababu tumekuja.

**33. Charlie:** Kwa ufupi ni wapi tunaweza kupata mafunzo ya dharura na ya uhakika kuhusu uandishi wa habari?

**34. Sister P:** Kwa hivyo bora tuzungumzie suala hili kwanza kabla ya kutembelea studio. Tunakubaliana?

**35. All:** Sawa!.

**36. Ezra:** Kwanza kabisa kabla ya kuanzisha stesheni ,ni lazima kubainisha ajenda kamili na kutambua wasikilizaji wenu.

**37. Young J:** Tayari tunafahamu hilo.

**38. Sister P:** Kwa ufupi tumechoshwa na stesheni ya ya taifa. Tumechoshwa na vipindi na muziki unaochezwa kila mara katika stesheni.

**39. Charlie:** Kwa kusisitiza anavyosema sister P ,kikundi chetu cha Dot.Com.Club, punde tu kimemaliza kurekodi Album yake. Ukipata nafasi labda unaweza kusikiliza hii CD. Tulipeleka katika stesheni hiyo ya taifa lakini hadi kufikia sasa hatujasikia ikichezwa. Kwa hivyo wakati tutakapoanzisha stesheni yetu ,tutaweza kucheza muziki wetu wenyewe utakao walenga vijana kama wewe,wa wengine wa kizazi cha sasa.

**40. Ezra:** Samahani lakini kama lengo lenu ni kuanzisha stesheni ya redio kwa misingi hiyo, sidhani mutafaulu.

**41. Young J:** Kwa nini?

**42. Ezra:** Mukitaka kuanzisha redio ya kijamii, kwanza ni lazima mujue malengo ya stesheni hiyo na maadili munayotaka kukuzwa miongoni mwa jamii hiyo. Burudani ni zuri lakini ni lazima mpanue mawazo yenu zaidi . Kwa mfano wakati stesheni hii ilipoanzishwa, madhumuni yake hasa ilikuwa kuwapa nafasi wanafunzi wanaosomea uandishi wa habari chuoni ili kufanikisha malengo yao katika taaluma hii, na pia kuelimisha jamii inayoishi karibu kuhusu masuala ya afya,mazingira,haki za

binadamu,masuala ya sheria na cha msingi kuboresha maisha yao.

**43. Sister P:** Sasa nimeelewa , Ezra, nadhani halitakuwa jambo la busara kuanzisha stesheni kucheza muziki tu mchana kutwa usiku kucha.

**44. Charlie:** Mbali na vipindi ni yapi mengine tunayoweza kufikiria?

**45. Ezra:** Suala jingine munalopasa kuzingatia ni mahala palipo na usalama wa kutosha kufungua ofisi, ambako munaweza kujenga studio zenu bila ya hofu ya vifaa vyenu kuibiwa au kuharibiwa.

**46. Young J:** Sister P, Je unayaandika hayo au niyaandike.

**47. Sister P:** Sote tunapasa kuyaandika. Kwa hivyo unachomaanisha ni kwamba studio hii si lazima iwe ya gharama sio?

**48. Ezra:** Ndio maanake, kimsingi, ni hamuna pesa za kutosha, na munachohitaji ni vifaa vya kimsingi kuanzisha studio hiyo. Hamuhitaji vifaa vya ghali kama vile vinavyotumika katika vituo vya televisheni au filamu.

**49. Charlie:** Kimsingi tunahitaji vifaa vya aina gani ?

**50. Ezra:** Munahitaji vifaa vitakavyotoa sauti nzuri na mashini zinazoambatana na vifaa hivyo.

**51. Young J:** Na tutajuaje vifaa hivyo Ezra?

**52. Ezra:** Hilo lisimjalishe. Nitawapa ushauri ufaao. Na kisha ni lazima muhakikishe laini zenu za simu ni barabara kabisa na pia muunganishwa na mtandao wa Interneti madhubuti .

**53. Sister P:** Mimi hupendelea vipindi vya mahojiano kupitia laini za simu, kwani kupitia njia hiyo unaweza kupata maoni ya watu wengi.

**54. Charlie:** Ni jmbo la kuvutia lakini mara nyingine unaudhika tu, hasa wakati unapokuwa unazungumzia suala nyeti kama vile ukame na uhaba wa chakula, halafu ghafla mtu anapiga simu kuzungumzia penzi lililovurugika

**55. Ezra:** Hayo ni mambo ya kawaida huwezi kuyaepuka katika sekta hii ya utangazaji hasa redio  Hii ndiyo sababu munahitaji mafunzo ya uandishi wa habari.Itampa fursa ya kuweza kukabiliana na changamoto hizi zinapotokea. Pia munafunzwa jinsi

ya kuwa waajibikaji na kuandika habari zisizoegemea upande wowote.Lakini zaidi namna a kuwachemsha wasikilizaji wako, masuala ya utafiti na mambo mengi tu.

**56. Charlie:** Ndilo swali nilitaka kukuuliza, wapi mtu anaweza kupata mafunzo ya uandishi wa habari?

**57. Ezra:** Unaweza kupata mafunzo haya kwa kujiunga na chuo kikuu kama mwanafunzi wa kawaida kama mim, au kusomea kozi fupi tu zinazotolewa hapa chuoni na taasisi nyingine za mafunzo ya uandishi..

**58. Sister P:** Kwani hatuwezi kujifunza kazini?

**59. Ezra:** Unaweza, lakini pia utahitaji muongozo kutoka kwa mtu aliyehitimu na ujuzi kutoka chuo kinachoheshimika. Je tayari mumepanga bajeti yenu?

**60. Young J:** Tatizo jingine hilo..!. mumesekia wenzangu. Ezra kabla ya kuuliza swali hilo kwanza nieleze kituo hiki kiligharimu pesa ngapi?

**61. Ezra:** Tuseme **Y**uro 7,000 hivi.

**62. Sister P:** Yaani unahesabu yuro elfu 1, 2,3,4,5,6, hadi SABA ?... Tutazipata wapi pesa hizo?

**END OF EPISODE**

**OUTRO**

Na hapo ndipo tunapofika mwisho wa kipindi cha leo kuhusu sekta ya habari na vyombo vya habari. Matumaini yangu ni kamba umeufuaria mchezo huu huku nikiraji kwamba utaungana nasi tena katika kipindi kijacho ambapo Young J na wenzake wameanza harakati za kutafuta fedha kufadhili mradi wao.

Pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu wa Dw- world.de / l b e. Ukiwa na maoni pia usisite kututumia hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!